**SEHEMU YA KWANZA.**

**1:0 JINA, NA MAWASILIANO YA KIKUNDI.**

Jina la kikundi; Kikundi hiki kitafahamika kama EX-CASFETA USHIRIKA,

1.1 Kikundi kilianzishwa 6/03/2015

1.2 Idadi ya wanachama ni ……Me ….. ke ….

1.4 Barua pepe ya kikundi……………

**1.2 MALENGO YA KIKUNDI.**

Kikundi kina malengo mbalimbali;

a. Kudumisha Umoja,Ushirikiano, Mshikamano Miongoni mwa WanaCASFETA waliowahi kusoma Chuo kikuu cha ushirika Moshi kwa Miaka Mbalimbali
b. Kujengana, Kuimarishana na Kutiana Moyo Kiroho, Kimwili, Kiuchumi, kitaaluma kwa Kupitia Programu mbalimbali ndani ya Kundi.
c. Kushirikiana kwa pamoja kwenye Matukio ya Kijamii kama vile Misiba na Harusi kwa kuzingatia utaratibu wa Kikundi.
d. Kuwezesha (Pesa, Ushauri na Vitu) Huduma ya Mikutano ya Nje ya injili (OGM) inayoratibiwa na CASFETA TAYOMI Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi.
e. Kutoa misaada ya Kijamii kwa Makundi Maalumu kwenye Jamii kama vile Watu wenye Ulemavu, Watoto Yatima na Wazee.

**3.0 MASUALA YA UANACHAMA**

**3.1 SIFA ZA MWANACHAMA**

a. Lazima Mwanachama awe amewahi kuwa Mwana Casfeta Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi.
b. Awe na Akili timamu
c. Awe na Umri wa kuanzia miaka 18
d. Akubaliane na Katiba na Miongozo yote ya Kundi.
e. Awe Msikivu na Mtiifu
f. Awe Mshiriki hai kwenye mambo yote yanayoendelea kwenye Kundi.

**3.2 UKOMO WA MWANAKIKUNDI.**

Uanachama utakoma kwa sababu zifuatazo.

a. Kifo
b. Kujiondoa au kuondolewa kwenye Kundi la WhatsApp
c. .Ukomo wa Mwanachama, utakoma pale ambapo Mwanachama atashindwa kushiriki Programu za kikundi kwa Muda usiozidi Miezi mitatu mfululizo bila taarifa yoyote.

d. Kutenda makosa yaliyo kithiri kama vile, kutoa siri za Kundi, kusababisha mgogoro au migogoro ndani ya Kundi.

**3.3 WAJIBU WA MWANAKIKUNDI.**

Mwanakikundi atakuwa na wajibu ufuatao.

a. Kushiriki katika shughuli zote zitakazofanyika kwenye kundi.
b. Ana wajibu wa kuchangia na kushiriki michango yote ya Harusi, Ugonjwa,Misiba itakayofanyika kwenye kundi.
c. Ana wajibu wa kuchangia na kushiriki Michango ya OGM.
d. Kuhudhuria vipindi vyote ,Mikutano, Vikao ,Ibada & semina bila kukosekana.
e. Wajibu wa kuheshimu mawazo ,maoni na mapendekezo ya Watu wengine kwenye kundi
f. Wajibu wa kutunza siri na taarifa za Kundi na wana kikundi wengine.
g. Wajibu wa kukusanya na kusimamia michango kwenye Kundi kama itakavyoelekezwa na Viongozi.

**3.4 HAKI ZA MWANA KIKUNDI**

a. Mwana kikundi atakuwa na haki ya kuchangiwa endapo akiwa na ,
    i. Harusi
    ii. Msiba – Mume ,Mke, Baba Mzazi, Mama Mzazi, Mlezi kutoka Utotoni, Mtoto wa Mwanachama na Mwanachama Mwenyewe.
    iii. Kupatwa na Ugonjwa Mkubwa utakaohitaji msaada wa wanakinundi; hili litajadiliwa na Viongozi na kuwasilishwa kwa wanakikundi kutoa maoni yao
b. Haki ya kupata au kupewa taarifa za shughuli mbalimbali za kikundi
c. Haki ya kuchagua au kuchaguliwa kuwa kiongozi

**3.5 UTARATIBU WA KUMCHANGIA MWANACHAMA**

Kikundi kitashiriki kumchangia mwanachama kwa kuzingatia historia(kumbukumbu) ya uchangiaji wake kwenye michango ya wengine kwenye kikundi.

**3.6 SHUGHULI AMBAZO KIKUNDI HAKITAFANYA.**

Ni Pamoja na;

a. Kikundi hakita shiriki & Kumchangia Mchango wowote mwanachama ambaye huwa hashiriki kwenye michango ya watu wengine.

b. Kikundi hakito changia michango ya rambi rambi kwa ndugu wengine wa Mwanachama isipokuwa Baba,Mama, Mtoto wa mwanachama na mwana kikundi mwenyewe. Rejea Kipengele (3.4 i,ii,ii)
c. Kwa mujibu wa Katiba hii kikundi hakita zurumu haki ya Mwanachama kama anastahili, na ikiwa hivyo Mwanachama ana haki ya kuwasilisha malalamiko yake kwa viongozi ili kupata msaada.

**SEHEMU YA PILI.**

**2.0 UONGOZI NA MUDA WA UONGOZI**

**a.** Kikundi kitakuwa na Uongozi utakao chaguliwa au kuteuliwa na Wanachama , Uchaguzi wa viongozi utafanyika kila baada ya mwaka mmoja na Kwa kupigiwa kula na 2/3 ya wanachama hai

**2.1 KAMATI TENDAJI YA KIKUNDI**

Kamati tendaji itakuwa na viongozi wafuatao

i. Mwenyekiti wa kikundi
ii. Katibu wa kikundi
iii. Mhazini wa kikundi
iv. Wajumbe

**2.2 KAZI YA KAMATI TENDAJI.**

Kamati tendaji itawajibika kwa kazi zifuatazo.

i. Kufanya tathmini ya utekelezaji wa mipango ya shughuli za kikundi.
ii. Kupanga mipango ya maendeleo na kuhakikisha Ustawi wa kila mwana kikundi Kiroho, kimwili, kiuchumi na Kitaaluma
iii. Kusimamia mapato na matumizi ya Fedha na kudhibiti ipasavyo
iv. Kuendeleza yote yaliyo azimiwa na wanakikundi wenyewe.

**2.3 SIFA ZA KIONGOZI.**

Kiongozi atakaye chaguliwa au kuteuliwa ni lazima awe na sifa zifuatazo.

- Ameokoka
- Mwaminifu
- Mvumilivu
- Mtunza siri
- Muwajibikaji
- Mtenda haki
- Awe muwazi

- Awe msema kweli
- Awe tayari kukosolewa
- Asiwe mtu wa kupenda makundi na kugawa wanachama.
- Awe tayali kushauriwa
- Asiwe mtu wa kutumia mabavu kulingana na nafasi yake
- Daima awe msuruhishaji wa migogoro inayo jitokeza.
- Awe mtu wa kujiheshimu kwenye jamii

**2.4 WAJIBU WA VIONGOZI.**

**A. MWENYEKITI**

Atakuwa na wajibu ufuatao.

- Ndiye msemaji wa kikundi
- Ndiye ataitisha na kuendesha vikao vyote vya kikundi.
- Atasimamia shughuli zote za kikundi
- Atawakilisha kikundi katika vikao vya nje ya kikundi.
- Atahimiza na kufuatilia maamuzi ya vikao vyote.
- Atahamasisha umoja katika kutoa michango na utendaji wa shughuli za kikundi.

**B. KATIBU**

Atakuwa na wajibu ufuatao.

- Ndiye mtendaji mkuu wa kikundi
- Ndiye mtunzaji kumbukumbu zote za kikundi
- Ndiye mwandishi wa mihutasari ya vikao vya kikundi
- Atakaimu nafasi ya mwenyekiti kama mwenyekiti hayupo
- Atatoa taarifa ya utekelezaji wa maazimio mbalimbali kwa mkutano wa wanakikundi wote.

**C. MHAZINI**

Atakuwa na wajibu wa ;

- Ndiye mtendaji wa masuala yote yahusiyo Fedha.
- Atakusanya na kutunza fedha zote za kikundi kwa muda kabla hazijapelekwa kunako husika.
- Atatunza kumbukumbu zote zinazo husu mapato na matumizi ya kikundi

**D.WAJUMBE**

Wajumbe watatoka kwenye kila mwaka wa wahitimu ili kupata uwakilishi mzuri **.**

Majukumu yao yatakuwa ni.

- Kutunza, kusimamia na kulinda nidhamu ya kikundi.
- Kulinda sheria na kanuni za kikundi
- Kutoa ushauri na mapendekezo itakapohitajika

**SEHEMU YA TATU**

**3. MASUALA YA UENDESHAJI, UTARATIBU WA MICHANGO NA MFUKO WA KIKUNDI.**

Uendeshaji wa kundi utakuwa ni kwa njia ya mtandao (online) whtsapp kwasababu wana kikundi tupo Mikoa mbalimbali na wengine nje ya Nchi

**3.1 UTARATIBU WA MICHANGO**

Kiwango cha Chini cha Kuchangia kwa kila mwana kikundi kwenye mchango wowote *utakaofanyika* Kwenye kikundi itakuw*a* ni 5,000/= Elfu Tano tu na zaidi ya hapo Mtu atatoa Kadri atakavyoguswa kuchangia.

Kwa wana kikundi ambao ni Wanandoa (Mr na Mrs) Watachangia Kiwango cha Chini Kuanzia 10,000/= (Elfu kumi tu) Na Zaidi ya hapo watatoa Kadri watakavyoguswa kuchangia. Na Endapo wanakikundi ambao ni wanandoa wakitoa Mchago kuanzia 5,000/= itahesabiwa kuwa Mwana kikundi mmoja ndiye aliyechangia siyo wote wawili.

**3.2 MAPATO NA MATUMIZI**

Taarifa ya Mapato na matumizi ya mfuko wa kikundi itasomwa kila baada ya mwaka mmoja.

**3.3 MFUKO WA KIKUNDI**

Kikundi Kitakuwa na Mfuko wa kikundi Utakaotokana na Asilimia 10 ya Kila Mchango utakaokusanywa kwenye Kikundi isipokuwa Mchango wa OGM tu huu utawasilishwa bila kukatwa asilimia 10.

**3.4 AKAUNTI YA KIKUNDI**

Kikundi kitakuwa na akaunti ambayo itatumika kutunzia Pesa za Kikundi Chini ya Usimamizi wa Mwenyekiti, katibu , mhazini na Mjumbe mmoja.

**3.5 FAIDA AU KAZI ZA MFUKO WA KIKUNDI**

Mfuko wa kikundi utakaopatikana kutokana na asilimia kumi (10%) ya kila mchango utakaokusanywa, utakuwa na majukumu na faida zifuatazo kwa wanachama na kikundi kwa ujumla:

a. Kusaidia Katika Mambo ya Dharura:

Mfuko huu utatumika kutoa msaada wa haraka kwa wanakikundi wanaokumbwa na changamoto za dharura kama vile  ajali, au matatizo ya kiafya.

b. Kuwa Akiba ya Kikundi:

Mfuko utakuwa ni hazina ya akiba ya kikundi ambayo itasaidia kugharamia shughuli mbalimbali za kikundi bila kutegemea michango ya papo kwa papo.

c. Kuwezesha Nauli kwa Wawakilishi:

Mfuko utatumika kugharamia nauli au usafiri wa mwakilishi au wawakilishi wa kikundi watakaoteuliwa kuhudhuria matukio au shughuli zinazomhusu mwanakikundi au wanakikundi.

d. Kusaidia Uendeshaji wa Shughuli nyingne za  Kikundi:

Mfuko utatumika kusaidia mipango ya maendeleo ya kikundi kama vile semina, miradi ya pamoja yenye manufaa kwa wanachama wote.

**3.3 MSIBA**

a. Wahusika wa rambirambi katika msiba watakuwa.
- Baba
- Mama
- Mke
- Mume
- Mtoto
- Mlezi kutoka utotoni.
- Mwanakikundi mwenyewe.

b. Mfiwa au Mwanakikundi aliyekaribu nae atatoa taarifa kwa Uongozi wa kikundi ndani ya masaa 24. Wanakikundi watapewa taarifa na watatakiwa wachangie mchango wa msiba ndani ya muda utakaowekwa, kila Mwanakikundi atapaswa kuchangia kiasi  cha kuanzia 5,000/= na Kuendelea.

**3.4 HARUSI**

a. Wahusika wa harusi watakuwa ni
- Wana  kikundi
- Mwana kikundi
- Mtoto

b. Mhusika atatoa taarifa kwenye uongozi wa kikundi ndani mwezi mmoja kabla. Wanakikundi watapewa taarifa na watatakiwa wachangie mchango wa Harusi ndani muda utakaowekwa na viongozi,  kila mwanakikundi atapaswa kuchangia kiasi cha kuanzia 5,000/= na Kuendelea . Rejea kipengele Na.(3.5(a)i )

### 3.5 OUTREACH GOSPEL MISSION (OGM)

a. Kila mwana kikundi anao wajibu wa kutoa sadaka (Mchango) wa kwenda kuhubiri injili kupitia huduma ya OGM inayoratibiwa na CASFETA TAYOMI CHUO KIKUU CHA USHIRIKA MOSHI. Pia kwa Mwanakikundi anayetamani kwenda kushiriki mkutano huo anaruhusiwa kwenda kushiriki kwa kutoa taarifa kwa uongozi wa EX-CASFETA ili kujua idadi ya washiriki katika mkutano huo.
b. Viongozi wa OGM watatakiwa kutoa taarifa kwa Uongozi wa kikundi mara tu baada kupata eneo la kwenda kuhubiri & Kupitisha bajeti ya mkutano. Wanakikundi watapewa taarifa na Uongozi na watatakiwa kuchangie mchango wa OGM ndani ya muda utakaowekwa.

### 3.6 TAARIFA NA UTUNZAJI WA KUMBUKUMBU

Kumbukumbu zote zita tunzwa kwa viongozi wa kikundi.

Taarifa zote za kikundi zitakuwa zinaandaliwa na Katibu na Mhazini wa kikundi ,taarifa hizo ni kama zifuatazo Wanachama,Rambirambi(Msiba) ,Harusi ,OGM,mapato & matumizi na michango mbalimbali.

### 3.7 UTARATIBU WA KUSHUGHULIKIA MALALAMIKO NA KUTATUA MIGOGORO

- Viongozi wataunda kamati ikiwa kuna mgogoro umejitokeza.

Kamati ya kushughulikia migogoro itakuwa na majukumu yafuatayo;

i. upokeaji wa malalamiko.
ii. kushughulikia migogoro.
iii. Utoaji wa mrejesho kwa mlalamikaji au walalamikaji.
iv. utunzaji wa kumbukumbu za malalamiko na utatuzi wake.

Aidha kama mgogoro au migogoro itaendelea miongoni mwa wanachama uongozi utaomba msaada kutoka kwa Wachungaji / Walezi wa Kiroho kwa ajili ya msaada Zaidi.

## SEHEMU YA NNE

### 4.0 MENGINEYO

### 4.1 MAREKEBISHO YA KATIBA

Marekebisho ya katiba yatafanyika endapo kutakuwa na haja ya marekebisho baada ya kukubaliwa na theluthi mbili (2/3) ya wanachama wa kikundi.

### 4.2 SEMINA, IBADA, MAOMBI, MIDAHALO NA MAJADILIANO

Viongozi wataweka Utaratibu maalumu wa kufanya Semina, ibada za pamoja, Maombi, Midahalo na majadiliano kwa njia ya Mtandao WhatsApp, Zoom na Kukutana kwa Pamoja kila itakapowezekana.